JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA 2023

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu:**

**Mkuu wa Shule:0756275058/0620245748**

**Makamu Mkuu wa Shule:0766736118/0735736118**

**Matron/Patron: 0769239090**

**SHULE YA SEKONDARI KIPETA,**

**S.L.P 78,**

**SUMBAWANGA.**

**Tarehe: 1.4.2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………….**

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIPETA HALMASHAURI YA SUMBAWANGA MKOA RUKWA MWAKA 2024.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya HGL AU HGLi kadri wizara itakavyopangwa.

Shule ya Sekondari KIPETA ipo umbali wa Kilometa 176 Mashariki mwa Mji wa SUMBAWANGA. Usafiri wa basi kutoka mjini SUMBAWANGA unapatikana katika kituo cha mabasi KATUMBA Nauli ni Shilingi 20,000/= kwa wanafunzi wanaotokea KIGOMA, TABORA NA KANDA YA ZIWA VICTORIA. Wanafunzi wanaotokea njia ya MBEYA kuelekea Dar-es-salaam magari yanapatikana standi ya mabasi Mbeya yameandikwa MBEYA-KILYAMATUNDU AU MBEYA KAMSAMBA nauli ni Tshs. 15,000/= na Wanafunzi wanaotokea mkoa wa SONGWE usafiri wao unapatikana standi ya mabasi MLOWO na mabasi yao yameandikwa MLOWO-KILYAMATUNDU AU MLOWO-KAMSAMBA nauli yao ni TSHS. 10,000/=. Ukifika Kilyamatundu nauli ya kwenda Shule ya sekondari Kipeta ni Tshs. 1,000/= tu kwa pikipiki.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 1.7.2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 30.6.2024. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 7.7.2024.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.0 Sare za shule

i) Sare ya shule hii ni suruali mbili (damu ya mzee na dark-blue) mashati mawili meupe mikono mirefu kwa wavulana. Sare ya michezo kwa shule hii ni bukta 2 rangi ya blue na tracksuit pair moja kwa wavulana.

ii) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

iii) Soksi jozi mbili Nyeusi za shule.

iv) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.

v) Sweta pair 2 (damu ya mzee 1 na darkblue 1) – ingawa siyo lazima kwa sababu kuna joto.

vi) Nguo za kushindia (shamba *Dress*) suruali 1 kijani kibichi na T-shirt ya kola (form six) ya blue yenye kola nyeupe na ufito mweupe mwishoni mwa mikono au T-shirt 1 ya blue ya round kola.

vii) Tai 2 ( dark blue 1 na damu ya mzee 1)

**2.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari counterbooks 14 (*4 quire* );
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi ya HGL, HGLi NA GENERAL STUDIES (History 1&2, English language 1&2, Literature in English na Geography 1&2. Kila somo kitabu kimoja yaani paper 1 kimoja na paper 2 kimoja na vitakaguliwa.
iv. Scientific Calculator;
v. Godoro 1 foot mbili na nusu
vi. Mashuka Jozi 2 ya pink, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1.
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. Kwanja 1 na jembe 1 kwa wanafunzi wa HGL na reki 1 na mifagio 2 ya ndani na nje kwa wanafunziHGLi

**2.2 Michango mbalimbali:**

**Kwa kuwa wanafunzi wote wanakaa bweni michango yao itakuwa kama ifuatavyo:**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**3.0 Sheria na Kanuni muhimu za Shule:**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha,

inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi**

**kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBUNI SANA SHULE YASEKONDARI KIPETA.**

**Saini ya Mkuu wa Shule:**

**Jina la Mkuu wa Shule: DELIGO PAUL LUPOLA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule:**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KIPETA
S.L.P.78 SUMBAWANGA

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0756275058/0620245748**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0766736118**
- **Mwandamizi Taaluma 0755090303**
- **Mwandamizi Malezi 0769239090.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MEDICAL EXAMINATION FORM 2024**

**KIPETA HIGH SCHOOL**
**P.O. BOX 78,**
**SUMBAWANGA.**

**DATE**………………………

MEDICAL OFFICER
…………………………………………
…………………………………………
…………………………………………

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR…………………………………**
**(NAME OF STUDENT)**

Please examine the above named as to his/her fitness as indicated below. Arrange the necessary treatment so that the certificate may be brought to school by the student.
This certificate must be signed by a qualified Medical Officer of a recognized Government hospital.

1. Hemoglobin …………………………………………………………………
2. P.V Blooding ………………………………………………………………..
3. (a) Blooding ………………………………………………………………...
   (b) Hearing ………………………………………………………………….
4. Blood pressure ……………………………………………………………...
5. Stool for routine examination ………………………………………………...
6. Urine for sugar ……………………………………………………………...
7. Skin diseases ………………………………………………………………..
8. Leprosy …………………………………………………………………….
9. Pulmonary tuberculosis ……………………………………………………
10. Asthma …………………………………………………………………….
11. Epilepsy …………………………………………………………………..
12. Deformity …………………………………………………………………
13. Mental problem …………………………………………………………
14. Comment……………………….………………………………. ………………

Name of medical officer……………………… Signature……………… Date……………

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA

SHULE YA SEKONDARI KIPETA

FOMU YA MZAZI KUKUBALI MWANAO KUJIUNGA NA SHULE

(Ikabidhiwe shuleni wakati mwanafunzi anaripoti)

1. Mimi..............................................................................baba/mama/mlezi wa ..............................................................................ninayeishi wilaya ya ........................................................kata ya ....................................mtaa wa ........................................................nakubali mwanangu ajiunge na shule ya sekondari Kipeta katika mchepuo wa ..............................................
2. Mimi mzazi/mlezi wa kijana huyu naahidi kushirikiana nan walimu katika malezi ya mwanangu akiwa shuleni na hata nje ya shule. Kwamba ni wajibu wangu kama mzazi/mlezi kumhimiza mwanangu asome kwa bidii na kufuata sheria na taratibu zote za shule.
3. Kwamba nitalipa michango yote shule katika muda uliopangwa na kwamba kila mwisho wa muhula nitamtaka mwanangu anipe maendeleo yake kitaaluma na tabia.

Jina la mzazi/mlezi....................................................................................

Kazi yangu..............................................................................................

Mahali ninapofanyia kazi..........................................................................

Saini ya mzazi/mlezi..................................Tarehe.....................simu.............

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA

SHULE YA SEKONDARI KIPETA

FOMU YA MZAZI KUKUBALI MWANAO KUJIUNGA NA SHULE

(Ikabidhiwe shuleni wakati mwanafunzi anaripoti)

TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

Tafadhali jaza fomu hii kwa uangalifu na ikabidhiwe siku ya kuripoti shule.

Mimi..........................................................................mazazi/mlezi pamoja na mwanafunzi tumezisoma na kuzielewa na kuzikubali taratibu na sheria za shule ya sekondari Kipeta.

1. Jina la mzazi/mlezi......................................................saini..............................
2. Jina la mwanafunzi.......................................................saini............................
   Kata/kijiji atokacho.................................wilaya.....................................mkoa.....
3. Ndugu mwingine wa karibu:
   Jina lake...................................................................................................
   Kijiji/kata anayoishi.................................wilaya............................mkoa............
   Kazi yake..................................................................................................
   Anuani yake...............................................................................................
   Uhusiano...................................................................................................
   Namba ya simu..........................................email................................................

SAINI YA MWANAFUNZI..................................................TAREHE.......................